# HALMASHAURI YA WILAYA YA SERENGETI

Shule ya Sekondari Nyamoko,
S.L.P 156,
Mugumu Serengeti.

Kumb. Na. S.1708/JI/2021/01 14.12.2020

Mzazi/Mlezi wa ………………………………………….
S.L.P. ………………………………………………………...

Ndugu,

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI NYAMOKO KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2021.**

**1.0 UTANGULIZI**

Nafurahi kukuarifu kwamba mtoto wako amechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule ya sekondari Nyamoko kwa mwaka wa masomo 2021. Shule ya sekondari Nyamoko ipo umbali wa kilomita 12.5 Magharibi mwa mji wa Mugumu wilaya ya Serengeti. Muhula wa kwanza wa masomo utaanza tarehe 11/01/2021 saa moja asubuhi. Hivyo basi mtoto anapaswa kuripoti shuleni kuanzia tarehe 11/01/2021 kwa ajili ya usajili na kuanza masomo.

**2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA**

2.1 SARE ZA SHULE

A. WAVULANA

- Suruali mbili kitambaa damu ya mzee (namba moja) mshono ni mifuko miwili mbele na mmoja nyuma, suruali iwe na marinda mawili na upana wa chini ni (inchi18) na isiwe modo au pisto na ivaliwe kwa staha bila kukata kiuno.
- Shati mbili kitambaa aina ya tetroni mikono mifupi na iwe na mfuko mmoja kushoto kifuani.
- Mkanda mweusi usiokuwa na picha wala rangi, uwe wa ngozi.
- Soksi nyeusi, viatu vyeusi vya ngozi nyenye kamba na kisigino cha kawaida.
- Tai mbili damu ya mzee (kitambaa namba moja)
- Sweta damu ya mzee ifanane na kitambaa cha suruali , **Fulana ya kijivu** (inapatikana pia shuleni), raba nyeupe za michezo na truck suit nyeusi zenye ufito mweupe pembeni.

B. WASICHANA

- Sketi mbili kitambaa damu ya mzee (namba moja) mshono **rinda boksi isiyokuwa na v shape**, zishonwe kwa staha na ziwe na urefu wa kawaida chini kidogo ya magoti.
- Shati mbili kitambaa aina ya tetroni mikono mifupi zenye mfuko mmoja kushoto kifuani.
- Kama mwanafunzi anavaa hijabu, rangi ya hijabu ifanane na sare ya shule.
- Soksi nyeupe ndefu, zivaliwe kwa staha.
- Viatu vyeusi vya ngozi nyenye kamba na kisigino cha kawaida.
- Tai mbili damu ya mzee zifanane na kitambaa cha sketi.

2.2 Sweta damu ya mzee ifanane na kitambaa cha sketi , **Fulana yenye rangi ya gold** (zinapatikana pia shuleni), Raba nyeupe za michezo na **truck suit ya light bluu** yenye ufito mweupe pembeni.

2.3 VIFAA VYA MASOMO

- Madaftari makubwa (counter quire 3 au 4) 12, Rula 1, Bofa 1, Kalamu za wino na za risasi.
- Kamusi ya Kiswahili sanifu, kamusi ya kiingereza kwa Kiswahili na kamusi ya kiingereza English Dictionary).
- Rimu ya karatasi yenye ukubwa wa A4, itakabidhiwa wakati wa kuripoti.
- **Aje na kiti na meza kwani hapa shuleni havipo.**

2.3. VIFAA VYA USAFI.

Mwanafunzi anapaswa kuja na ufagio wa chelewa na jembe jipya lenye mpini.

## 3.0 SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya elimu namba 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria namba 10 ya mwaka 1995. Aidha shule inazingatia miongozo yote inayotolewa na serikali juu ya usimamizi na uendeshaji wa elimu hapa nchini.

3.1 SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

Zifuatazo ni sheria na kanuni muhimu za shule

a) Kuheshimu viongozi, walimu, wafanyakazi, wazazi, wanafunzi, na jamii.

b) Kuhudhuria shuleni na darasani kwa muhula mzima bila kukosa na kuzingatia ratiba ya shule

c) Kushiriki kwa umakini katika kufanya kazi za ziada baada ya vipindi.

d) kuwahi shuleni, kuhesabu namba na kufanya usafi wa nje na darasani bila kukosa.

e) kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya uwepo wako ndani ya mipaka ya shule wakati wote uwapo shuleni.

f) kuzingatia usafi wa mwili wako, mavazi na mazingira ya shule muda wote.

g) kuvaa sare ya shule muda wote uwapo ndani ya shule au hata nje ya shule utakapokuwa kwenye shughuli za kishule.

h) Kutunza mali za shule na umma kwa ujumla.

## 4.0 MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE

a) Uasherati, Ulevi na matumizi ya dawa za kulevya kama vile sigara, kokeini, mirungi, n.k
b) Kupiga ama kupigana
c) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma au mali ya mtu binafsi.
d) Kudharau bendera au wimbo wa taifa
e) Kupata au kusababisha ujauzito.
f) Kuoa au kuolewa.
g) Kutoa au kushiriki katika utoaji wa mimba.
h) Kugoma au kuchochea mgomo.
i) Kuongoza au kushiriki katika tendo lolote la kuvuruga amani ya shule au nchi.
j) Kukataa adhabu kwa makusudi.
k) Kumiliki au kutumia simu ya mkononi ndani ya eneo la shule bila kibali.
l) Makosa mengine ya jinai kama vile wizi, ubakaji n.k.

## 5.0 MAMBO MENGINE MUHIMU YANAYOPASWA KUKAMILISHWA

- Mwanafunzi anatakiwa afanyiwe uchunguzi wa afya (Medical examination) kabla ya kuripoti na awasilishe shuleni fomu husika (**kiambatisho C)** siku ya kuripoti.
- Mwanafunzi anatakiwa ajaze fomu ya kukubali kujiunga na shule (**kiambatisho A**) na kuiwasilisha shuleni siku ya kuripoti.
- Mzazi/mlezi anatakiwa ajaze fomu ya ahadi ya kushirikiana na uongozi wa shule (**kiambatisho B**) na kuiwasilisha shuleni siku ya kuripoti.
- Mwanafunzi aje na faili dogo (folder file) kwa ajili ya kutunzia kumbukumbu zake.
- Mwanafunzi anatakiwa aje na cheti halisi cha kuzaliwa na akabidhi shuleni nakala ya cheti hicho baada ya kusajiliwa.

Nakutakieni utekelezaji mwema

Wako,

**Joseph P. Kalomo**

**Mkuu wa shule**

**0765034674 au 0764067446**

HEADMASTER
NYAMOKO SEC. SCHOOL
MUGUMU/ SERENGETI

## KIAMBATISHO A

FOMU YA KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE

**(Ijazwe na mwanafunzi)**

Mimi …………………………………………Nimesoma sheria, kanuni na taratibu za shule mbele ya mzazi /mlezi wangu na kuzielewa. Ninaahidi kwamba nitakuwa mtiifu kwa uongozi wa shule kwa kuzingatia kanuni na taratibu zote kama zilivyoainishwa na kwamba sitashiriki katika matendo yoyote yanayoweza kusabababisha nifukuzwe shule.

Jina la mwanafunzi ………………………………Saini ……………......tarehe ………….

## KIAMBATISHO B

**(Ijazwe na mzazi /Mlezi)**

Mimi …………………………………….wa kata ya ………………………kijiji/kitongoji cha ……………………ambaye ni mzazi/mlezi wa mwanafunzi ………………………………wa kidato kwanza 2021 katika shule ya sekondari Nyamoko. Ninaahidi kwamba nitashirikiana na uongozi wa shule kumsimamia mwanafunzi huyu katika malezi bora, mahudhurio yake shuleni na kumpatia mahitaji yake ya msingi awapo shuleni na nyumbani. Pia nitamhimiza mwanafunzi kuzingatia kanuni na taratibu za shule ipasavyo.

Jina la mzazi/mlezi …………………………………….saini…………….tarehe……………

## KIAMBATISHO C

FOMU YA UCHUNGUZI WA AFYA (MEDICAL EXAMINATION FORM)

**(Ijazwe na mganga mkuu wa hospitali ya wilaya upande wa serikali)**

To medical officer,

…………………………………

P.O. BOX ……………………..

…………………………………

Dar sir/madam

RE: MEDICAL EXAMINATION FOR …………………………………… (Student's name)

Please examine the above named student to his/her physical and mental fitness for a full time study. The examination should include the under listed areas.

| | |
|---|---|
| 1. Eye site ………………………… | 6. Leprosy……………………………… |
| 2. Hearing ………………………… | 7. Epilepsy…………………………….. |
| 3. Limbs ………………………… | 8. Neurosis……………………………. |
| 4. Veneral diseases………………… | 9. Pregnancy…………………………….. |
| 5. HIV/AIDS…………………… | 10. Other serious diseases ……………… |

General comment: ……………………………………………………………………........................

Name: ………………………… Signature:………… Designation:……………date ……......

HEADMASTER
NYAMOKO SEC. SCHOOL
MUGUMU/ SERENGETI